**MUHTASARI WA HOTUBA YA MWENYEKITI KUHUSU RIPOTI YA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO YA BARAZA LA WAWAKILISHI,**
**ZANZIBAR.**

## 1. **UTANGULIZI**

**Mheshimwia Spika,** nianze kwa kumtanguliza aliyetuumba sisi wanadamu na viumbe vyengine na kutunuku muda huu uhai na afya njema iliyotuwezesha kukutana katika Baraza hili tukufu. Aidha, shukrani ziwe kwako Mheshimiwa Spika na Viongozi wengine wa Baraza kwa namna mnavyotuongoza na kutuwezesha kutimiza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi katika Baraza hili. Tunafarajika kwa mashirikiano ya dhati mnayotupatia katika Kamati yetu ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuendelea naomba nitambue ushirikiano mkubwa uliopelekea kufanikisha kazi hii ya Kamati kutoka kwa Wajumbe wa Kamati ambao wamefanya kazi kwa bidii na maarifa pasi na kuchoka. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mihayo Juma N'hunga — Mwenyekiti,
2. Mhe. Zawadi Nassor Salum — M/Mwenyekiti,
3. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma — Mjumbe,
4. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) — Mjumbe,
5. Mhe. Mohamed Ahmada Salum — Mjumbe,
6. Mhe Kombo Mwinyi Shehe — Mjumbe na

7. Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir Mjumbe.

Aidha, shughuli za Kamati hii zimekuwa zikiratibiwa na Makatibu wawili kutoka Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, ambao wametimiza wajibu wao ipasavyo katika kuhakikisha kwamba Kamati yetu inatekeleza majukumu yake. Makatibu hao wamekuwa ni msaada mkubwa kwa Kamati na chachu ya mafanikio ya Kamati hii kwani wamekuwa wakipokea kuchambua Kanuni zote zinazowasilishwa na kuwashauri Wajumbe namna bora ya kuzifanyia kazi Kanuni hizo na kufanikisha ukamilishaji wa Ripoti hii ninayoiwasilisha. Naomba nao niwataje kwa majina yao kama ifuatavyo:

1. Ndugu Karima Abdul-Wahab na

2. Ndugu Abdu Maulid Haji.

Aidha, Kamati inatambua mchango wa Afisa Sheria Shamail Abeid Khamis kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Utumishi na utawala bora ambaye alifanyakazi kazi na Kamati bega kwa bega katika kukamilisha kazi hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ni Kamati muhimu sana hasa kwa kuzingatia kuwa kazi ya msingi ya Baraza ni kutunga Sheria. Tunapozungumzia Sheria inajumuisha na Sheria Ndogo Ndogo ambazo kwa kuzingatia Masharti ya kifungu cha 79(6) madaraka hayo ya kutunga Sheria yamekasimiwa kwa Afisa au Taasisi nje ya Baraza (deligation).

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa kukasimu madaraka lazima kufuatane na usimamizi (Deligation and Supervision) hivyo Kamati yetu ndiyo yenye jukumu la kufanya kazi ya usimamizi kwa wale waliokasimiwa madaraka hayo kwa niaba ya Baraza. Hivyo Kamati hii inapokuwa katika kutekeleza majukumu yake inahakikisha kwamba misingi ya utungaji wa Sheria inazingatiwa na kufuatwa kikamilifu kwa kila Taasisi au Afisa aliyekabidhiwa jukumu la kutunga Sheria Ndogo Ndogo. Miongoni mwa mambo

yanayozingatiwa ni pamoja na kuhakikisha Sheria inayotungwa haikiuki misingi ya Katiba na pia Sheria hiyo iwe imepewa Mamlaka na haendi kinyume na Sheria Mama. Aidha, nyezo muhimu tunazotumia kama muongozo wa kazi zetu ni kuzingatia Sheria ya Tafsiri na Sheria ya Utumishi pamoja na Sheria ya Makosa ya Jinai. Kamati hutumia njia ya kukutana na walengwa wa Sheria ndogo ndogo zinazofanyiwa uchambuzi ili kupata hali halisi iliopo kuhusiana na Sheria husika.

**Mheshimiwa Spika,** matumizi ya rejea mbali mbali zilizoandikwa na wataalamu wabobezi pia huwa ni nyezo yetu inayotusaidia kufanya mapitio ya uandishi wa Kanuni hasa suala la utaalamu na mbinu za uandishi.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo naomba sasa nijikite katika kusoma muhtasari wa kilichomo katika ripoti ya Kamati kwa mwaka 2022/23, baada ya shughuli mbali mbali zilizotekelezwa katika kipindi hicho.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati katika kutekeleza majukumu yake imeendelea na kazi zake za mizunguko mitatu. Mzinguko wa Kwanza ulikuwa tarehe **07/03/2022** hadi **25/03/2022,** mzinguko wa Pili tarehe **11/07/2022** hadi **29/07/2022** na mzinguko wa Tatu tarehe 3/10/2022 hadi tarehe 21/10/2022 na mzunguko wa Nne tarehe 19**/12/2022** hadi **06/01/2023**

## 2. **MADHUMUNI YA RIPOTI**

**Mheshimiwa Spika,** Muhtasari huu unakusudia kueleza madhumuni ya Ripoti ya Kamati ambayo ninavyoamini kila Mjumbe ameipata na amepata muda wa kutosha wa kuipitia ili kuweza kuisaidia Kamati kupata maoni ya Wajumbe na hatimae kuimarisha zaidi Ripoti hiyo. Kwa ujumla Ripoti inakusudia kueleza kwa kina yale yaliobainika katika utendaji kazi wa Kamati kwa kupitia Kanuni na kubainisha mafanikio na

changamoto zinazokabili Kamati huku tukiamini changamoto hizo zinaweza kutatuka

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeweza kutekeleza yale yote yalioainishwa katika ripoti kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 107 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi ambazo zimeainisha majukumu ya Kamati katika Jadweli la Kwanza la Kanuni hizo. Aidha, Ripoti ya Kamati imeainisha kiukamilifu majukumu hayo.

**Mheshimiwa Spika,** njia mbali mbali zimetumika kufikia malengo ya Kamati. Miongoni mwa njia hizo ni:

- Kupitia nyaraka ambazo Kamati ilikusudia kuzifanyia kazi
- Kufanya mahojiano na Maafisa wanaohusika na Kanuni hizo.
- Kufanya Ziara katika Taasisi ambazo Kanuni au Sheria Ndogo Ndogo hizo zinatumika ili kuweza kubaini mafanikio na changamoto zao katika utekelezaji wake.

Baada ya Kamati kupokea Kanuni hizo na kuzifanyia mapitio zilijitokeza baadhi ya changamoto kama vile, Kanuni nyingi kuwa zimeandikwa kwalugha ya kiengereza. Suala hili limekuwa likijirejea licha ya kwamba Kamati ilishatoa maelekezo kwa Taasisi na Wizara pia kwa kupitia Ripoti ya Kamati iliyopita ilielekeza suala hilo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Kanuni nyingi hutungwa na mawaziri ambao wote ni Wajumbe wa Baraza lako Kamati inawaomba tena kuzingatia matakwa ya Katiba na Sheria na huo sio utashi wa Kamati ili kuhakikisha Kanuni zinawasilishwa kwa lungha ya Baraza ambayo ni lugha ya Kiswahili. Aidha, matumizi ya lugha ya Kiswahili katika uandishi wa Kanuni yatasaidia uwelewa kwa walengwa na watumiaji wa Kanuni husika ambao wengi wao ni watumiaji wa lugha ya Kiswahili

**Meshimiwa Spika,** Kanuni zote zilizowasilishwa kwa Lugha ya Kiengereza Kamati haikuweza kuzifanyia kazi na kuzirejesha

katika Taasisi husika. Ni imani ya Kamati wale wote waliowasilisha Kanuni kwa Lugha ya Kiengereza watazingatia maelekezo ya Kamati. Ili kuona kwamba wamezingatia masharti ya Katiba na Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Rejea: Kifungu cha 87 cha Katiba ya Zanzibar, 1984 na *Kanuni ya 25 ya Kanuni za kudumu za Baraza la Wawakilishi).*

**Meshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba Taasisi nyingi haziko tayari kuwasilisha Kanuni zao kwa Kamati, jambo hii lilipelekea Kamati hii kutumia jitihata za ziada kuziitisha Kanuni hizo kwa kutumia uwezo wa Kamati kupitia Kanuni ya Baraza. Aidha, Kanuni zote zilizowasilishwa katika Kamati baadhi yao zilikuwa na kasoro nyingi na kupelekea baadhi ya Kanuni kufutwa kutokana na kutokidhi viwango vya uwandishi. Vile vile, baadhi ya Kanuni zilibainika kuwa na marekebisho mengi hadi kupoteza uhalisia wa Kanuni zenyewe,

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni zilizochapishwa kwa lugha ya kiswahili na kuwasilishwa Barazani kwa mwaka 2022 na kufanyiwa kazi kama ifuatavyo;

**1.** Kanuni za Usafi na Adhabu za Papo kwa Papo, 2021

**2.** Kanuni za Mwenendo wa Mahakama ya Kadhi, 2021

**3.** Kanuni za Utumishi za Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), 2021

**4.** Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, 2007 (pamoja na marekebisho ya 2017)

**5.** Kanuni za Utumishi za Shirika la Bima Zanzibar, 2017

**6.** Kanuni za Utumishi za Benki ya Watu wa Zanzibar, 2022

**7.** Kanuni za Utumishi za Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, 2016

**8.** Kanuni za Taasisi ya Viwango Zanzibar (Ada na Tozo),

2022

**9.** Kanuni za Ushuru wa Huduma za Baraza la Manispaa Mjini, 2022

**10.** Kanuni za Tozo za Huduma na Biashara za Baraza, 2022

**11.** Kanuni za Utumishi za Shirika la Bandari Zanzibar, 2012

Katika kuzifanyia mapitio Kanuni hizo Kamati ilitaka kujiridhisha juu ya hoja zifuatazo:

a. Utaratibu mzima uliotumiwa na Wizara au Taasisi katika kutunga Kanuni husika.

b. Sababu zilizopelekea kutungwa kwa Kanuni hizo.

c. Ushirikishwaji wa Wataalamu mbali mbali wa Ndani na Nje ya Taasisi.

d. Ushirikishwaji wa Wadau wanaohusika na Kanuni hizo.

e. Baadhi ya Kanuni Sheria zake ni za muda mrefu Kamati ilitaka kufahamu kwa nini zilichelewa kutungwa.

f. Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Sheria kabla ya kutungwa Kanuni hizo.

g. Kulikuwa na utaratibu gani uliotumika kabla ya kutungwa kwa Kanuni hizo na ulikuwa na upungufu gani. Je, Kanuni hizo zitaweza kuondoa kasoro hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Jukumu la msingi la Kamati kabla ya kufanya uchambuzi wa Kanuni au Sheria Ndogo Ndogo hulazimika kuipitia Sheria husika iliyotoa Kanuni hiyo pamoja na Kanuni husika ili kuhakikisha kuwa Kanuni hizo imetimiza

vigezo vya kisheria na kuangalia iwapo hakuna eneo lililoachwa pasi na kutungiwa Kanuni, huku Sheria ikihitaji kutungwa kwa Kanuni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika kutekeleza wajibu wake ilibaini kasoro kadhaa katika Kanuni hizo kama vile ***Makosa ya Kimuundo, Kimaana, Kiuchapaji, Kisarufi, kiuandishi na mgongano wa Kanuni na Kanuni nyengine au Sheria.***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia kasoro hizo na kupendekeza marekebisho. Hali hiyo ilipelekea baadhi ya Kanuni kuondolewa na kutakiwa kuandikwa upya kutokana na kasoro nyingi zilizojitokeza na kutokidhi vigezo vya kisheria vya Utungaji wa Kanuni. Mfano, Kanuni ya Utumishi ya Shirika la Utangazaji, Kanuni hii baada ya kupitia imebainika kuwa ni kama vile nakala au kivuli cha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya 2014, Kanuni haikuweza kuzingatia mambo mahsusi yanayohusu Shirika hilo na kufanya marejeo ya Kanuni ya Utumishi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika**, Pia, Kanuni imebainika kuwa na makosa mengi ya kiuandishi na kiufundi mfano mgongano wa Kanuni zaidi ya moja kueleza dhana moja hilo limejitokeza mara kadhaa katika kanuni hiyo. Aidha, Kanuni imetumia maneno mawili yanayoeleza dhana moja jambo ambalo halikubaliki kiuandishi. Vile vile Kanuni imeweka adhabu ambazo haina Mamlaka nazo.

**Mheshimiwa Spika**, kasoro nyengine ambayo imebainika ndani ya Kanuni hiyo kwamba kuna mkanganyiko wa majukumu baina ya Bodi na Kamati Tendaji. Hayo ni miongoni tu ya mambo yaliyopelekea Shirika kufikia uamuzi wa kuiomba Kamati kuridhia kuifuta na kuiandika upya kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, zipo Kanuni zimebainika kuwa hazikufuata Taratibu za Utungaji ikiwemo ushirikishwajiwa Wadau ili kupata

maoni yao. Mfano wa hizo ni Kanuni ya Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS). Kamati ilipata fursa ya kupitia Kanuni hiyo na iliona kuwa kuna haja ya kufanya Ziara katika Taasisi hiyo, katika Ziara hiyo ilibaini Utungwaji wa Kanuni hiyo ulikosa kuzingatia eneo muhumu la kuchukua Maoni ya Wadau kwani Wadau walishindwa kuelewa uwepo wa Kanuni hiyo. Hivyo, Kamati ilipendekeza kufanyiwa mapitio Kanuni hiyo na kuhakikisha Wadau wanashirikishwa na maoni yao yanazingatiwa ili kuweza kupatikana Kanuni iliyobora na yenye kiwango kikubwa cha ushirikishwaji wa Wadau.

Aidha baadhi ya Kanuni zimeonekana kupingana au kutafautiana na Sheria Mama jambo ambalo ni kosa kiuandishi kwani kwa utaratibu Kanuni haitakiwi kupingana au kutafautiana na Sheria. Mfano wa Kanuni hiyo ni Kanuni za Usafi na Adhabu za Papo kwa Papo, 2021

Katika **Kanuni ya Usafi na Adhabu za Papo kwa Papo, 2021**Tafasiri ya neno *Baraza* ni tofauti na tafasiri iliyotolewa na **Sheria Nam 7 ya 2014** ambapo Sheria imetafasiri neno Baraza kama Baraza lililoanzishwa kwa mujibu wa Sheria Mama na Kanuni. Hata hiyo, Kanuni imetafasiri Baraza maana yake ni **Baraza la madiwani ambalo limeanzishwa ndani ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa**. vilevile Mamlaka yaliyotolewa kwa Afisa Aliyeidhinishwa chini ya Kanuni ya 5(2) ya **Kanuni ya Usafi na Adhabu za Papo kwa Papo, 2021** ni zaidi ya Mamlaka ambayo ameidhinishiwa Afisa huyo ndani ya Sheria

**Mheshimiwa Spika**, kiuandishi hayo ni makosa na yanapaswa kuzingatiwa na kuekwa sawa ili kuondoa mgongano baina ya Sheria na Kanuni kwa watumiaji.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Kasoro za Kimantiki, baadhi ya Kanuni zililazimika kurudishwa kwa marekebisho au kuondolewa kabisa kutokana na kasoro za kimantiki.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kanuni huandikwa kutokana na nguvu inayopewa na Sheria Mama na haipaswi kwenda kinyume na dhana iliyopo katika Sheria Mama, kutofautiana huko kunapelekea kuibuka kasoro za kimantiki katika uandishi wa Kanuni. Miongoni mwa Kanuni hizo ni Kanuni ya Manispaa ya Mjini ambayo ilikiuka masharti ya kifungu kilichoipa Mamlaka ya Kutunga Kanuni hiyo. Hivyo kupelekea Kanuni hiyo kukosa nguvu kisheria na Kamati ilipendekeza kuondolewa Kanuni hiyo.

Aidha, kwa upande wa Kanuni ya Mwenendo wa Mahakama ya Kadhi nayo pia imeonesha kasoro za aina hiyo kwa mfano Kanuni imeshindwa kuainisha muda ambao mdaiwa anatakiwa kuwasilisha majibu ya madai na badala yake imeachiwa mahakama kuwa na uamuzi (discreationary power) jambo hilo ni hatari katika utafutaji wa haki kwani linaweza kutumika vibaya (Rejea Kanuni ya 9 na 11 ya Kanuni hizo)

**Mheshimiwa Spika,** hizo ni miongoni mwa Kanuni chache tu tulizoainisha hapa ambapo moja imekwenda nje ya mipaka ya kisheria na pia inagongana na Sheria nyengine na nyengine imeshindwa kuzingatia mwenendo bora na uliozoeleka katika taratibu za mwenendo wa Sheria za madai. Hivyo Kamati inashauri Viongozi wenye Mamlaka ya Kutunga Kanuni hasa mawaziri na wengine waliokasimiwa madaraka hayo kuhakikisha wanakuwa ndani ya mipaka yao wakati wanatunga Kanuni na sio vinginevyo, kwani kufanya hivyo katika dhana ya kisheria kunajulikana kama kufanya jambo nje ya mipaka *(ulravire)* na kunapeleke Kanuni hiyo kuwa batili tokea awali *(void abnitial).* Aidha kwa upande mwengine utungaji wa Kanuni zinazotofautiana na Kanuni nyengine katika dha ya jambo moja katika mamlaka moja (same jurisdiction) kunapelekea tuonekane kutokuwa na msimamo katika utaratibu wa uandishi wa Sheria zetu (double standard).

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu Makosa ya kimuundo, katika uandishi wa Sheria suala la kuzingatia Mtiririko na Muundo (logical sequence) ni muhimu na humsaidia mlengwa kuelewa dhana ya Sheria husika. Aidha, hupelekea kila chombo kupewa jukumu lake bila mgongano, katika kutekeleza jukumu lake Kamati ilibaini kuwa zipo Kanuni za baadhi ya Taasisi hazikuzingatia suala hilo na kupelekea mgongano wa kimajukumu kwa vyombo vya Taasisi hizo. Miongoni mwa Kanuni hizo ni Kanuni ya Utumishi ya Shirika la Bandari na Shirika la Utangazaji, ambapo mashirika hayo kwa sasa yapo katika utaratibu wa kuzifuta na kuziandika upya.

**Mheshimiwa Spika,** ukifanya marejeo katika Kanuni ya Shirika la Bandari katika sehemu inayohusu Muundo wa Kamati ya Uongozi utaona jukumu lake la msingi ni kusimamia nidhamu tu ambapo kimsingi sio jukumu pekee la Kamati hiyo ya Uongozi. Aidha, Wajumbe wa Kamati hiyo ni wengi mno na kuonekana kuwa ufanyaji kazi wa Kamati unakosa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Kanuni za Utumishi za Shirika la Utangazaji, Kamati imebaini majukumu ya Bodi kubebeshwa Kamati Tendaji, hii imetokana na kukosekana kwa mtiririko mzuri na mgawanyo wa majukumu kwa kila chombo cha Taasisi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika upande wa Makosa ya kiuchapaji na uandishi, Kanuni zote zilizofanyiwa mapitio na Kamati zimebainika kuwa asilimia kubwa zina makosa mengi ya kiuchapaji na kiuandishi jambo ambalo linaweza kupelekea kupoteza maana iliyokusudiwa na wakati mwengine kuweze kupelekea kumkosesha mtu haki zake au kumpa mtu haki asiyepaswa kupewa.

Kwa mfano Kanuni ya 80 ya Kanuni za Utumishi za Mamlaka za Viwanja vya Ndege imeweka Mamlaka ndani ya Kanuni kumpa Waziri Mamlaka ya kutunga Kanuni ambapo suala hilo sio sahihi

kwa Kanuni kutoa Mamlaka ya kutungwa Kanuni nyengine. Hivyo Kamati ilitaka kufahamu uwezo huo umetokana na Kifungu gani cha Sheria na ilikosa majibu. Hivyo, Kamati iliushari kufanyiwa marekebisho ya Kanuni hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kasoro nyengine ya kiuandishi ambayo imejitokeza katika Kanuni nyingi ni suala la uandishi wa Kanuni za adhabu kwani Kanuni nyingi zilivyoandi kwa zimempa mkosaji adhabu kabla ya kumtia hatiani jambo ambalo ni kosa katika uandishi. Aidha, yapo makosa ambayo tayari yameshazungumzwa katika Sheria nyengine Maalum na kuekewa adhabu zake jambo ambalo sio sahihi kurejea kwani linaweza kuleta mgongano wa kitaasisi. Miongoni mwa Kanuni hiyo ni Kanuni ya 89 ya Kanuni ya Utumishi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, ambapo Kamati ilishauri kufutwa Kanuni hiyo kwani zipo Sheria zinazosimamia ujinai wa masuala haya kwa mtu yeyote.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muhutasari huu hizo ni miongoni wa changamoto zilizojitokeza katika Kanuni zilizopitiwa na Kamati. Uchambuzi wa kina umeelezwa katika Ripoti kuu ambayo imegaiwa kwa kila Mjumbe.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika kukamilisha kazi zake ililazimika kufanya Ziara katika maeneo kadhaa ambayo yaliweza kuijengea Kamati uwelewa zaidi na hivyo kuweza kuishauri Serikali ipasavyo kutokana na kujifunza kutoka kwa wengine.

Miongoni mwa maeneo hayo ambayo Kamati ilifanya ziara ni:

1. Shirika la Utangazaji Zanzibar, Dar es Salam.
2. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Tanzania (NSSF).
3. Mamlaka ya Bandari, Dar es Salam.
4. Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege, Dar es Salam.
5. Kampuni ya Uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KADCO).

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya ziara hizi zilitokana na kazi

ya upitiaji wa Kanuni za Utumishi zinazohusiana na Taasisi zilizoainishwa hapo juu ili kuona wenzetu wanatatuaje changamoto zao kiutumishi katika utekelezaji wa Kanuni zao. Katika ziara hizo Kamati iliweza kuona hali halisi ya Taasisi ambazo Kanuni zake zilikuwa zinafanyiwa mapitio na Kamati. Kamati iliweza kuzishauri Taasisi ipasavyo na kupendekeza baadhi ya marekebisho kwa Kanuni hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijifunza mengi kutoka Mamlaka ya Bandari Tanzania na Viwanja vya ndege vya Kimataifa vya Julius Nyerere na Kilimanjaro.

Miongoni mwa mambo yaliopelekea kufanya ziara Mamlaka ya Bandari Tanzania baada kupitia **Kanuni za Utumishi za Shirika la Bandari Zanzibar, 2012**. Watendaji wa Shirika hilo ambao ndio Wadau wa Kanuni hii waliainisha changamoto mbali mbali zilizomo katika Kanuni na zile ambazo zinatokea nje ya matakwa ya Kanuni. Baadhi ya changamoto hizo ni kama ifuatavyo;

i. Chama cha Wafanyakazi wa Bandari kutopata fursa ya kushiriki katika maamuzi yanayohusu utendaji wa Shirika

ii. Maslahi ya watendaji kutopatikana ipaswavyo kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, 2012

iii. Uwepo wa mgogoro kati ya uongozi wa Shirika na wafanyakazi wa kada za usafi na ulinzi ambao wanafanyakazi kwa malipo ya kila siku

iv. Kutokufahamika kisheria muingiliano kati ya Shirika la Bandari na Kampuni ya inayofanya kazi za usafi inayojulikana kama Jitihada njema.

Katika ziara yake Kamati iliona kuna tafauti kati ya Shirika la Bandari Zanzibar na Mamlaka ya Bandari Tanzania hasa katika utaratibu wa watumishi na uajiri wao.

Kuhusu suala la ajira za watumishi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania, Watumishi wake wapo wale wenye Mikataba ya Kudumu na Mikataba ya Muda Maalum na hakuna wafanyakazi wa kutwa ambao wapo chini ya Shirika moja kwa moja. Wafanyakazi wa kutwa wapo chini ya Kamapuni ambazo zimefunga Mikataba na Mamlaka. hali hiyo ni tofauti na Shirika ambapo wafanyakazi wa kutwa nao ni sehemu ya wafanyakazi wa Shirika kwa mujibu wa masharti ya Kanuni.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya ziara hiyo, naliomba Baraza lako lielewe kwamba Shirika limeanza hatua za awali za mchakato wa marekebisho ya Sheria na Kanuni ili Shirika liweze kupata ufanisi katika utendaji wake kupitia Sheria na Kanuni zake kwa Maslahi mapana ya Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilipata fursa kupitia Kanuni ya Utumishi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, 2016. Katika kupitia Kanuni hiyo mambo kadhaa yalizua mjadala, miongoni mwa hayo ni:

a) Wafanyakazi wanaofanyakazi katika mazingira hatarishi kama mionzi na waongoza ndege wamewekewa utaratibu maalumu wa stahiki zao.

b) Muda wa ziada kulipwa kwa utaratibu maalumu.

c) malipo ya likizo ya kawaida na ile ya uzazi, posho mbali mbali zimeainishwa vyema.

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara ya Viwanja vya ndege vya Julius Nyerere na Kilimanjaro Kamati ilibaini kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imepiga hatua ukilinganisha na viwanja vyengine tulivyotembelea katika masuala ya Utumishi. Hata hivyo Kamati inashauri Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kuangalia maslahi

ya watumishi kwa kuzingatia mifano ya viwanja vyengine tulivyotembelea na Mamlaka kuweza kufanya marekebisho ya Kanuni katika suala la maslahi kwa kadri itakavyonekana inafaa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upende wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Kamati ilifanya mapitio ya Kanuni ya ZSSF. Kabla ya kutoa ushauri wake Kamati iliona ni vyema kwenda kujifunza zaidi katika mfuko mwengine kama huo kutokana na umuhimu wa mfuko huo, Kamati ilifanya hivyo ili iweze kuishauri vyema taasisi husika. Miongoni mwa Mambo ambayo Kamati imejifunza ni kuwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii umeweke fao maalum la kuumia kazini. Hali hiyo ilichochea kasi ya marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar ili kuweka fao hilo. Ni imani ya Kamati kuwa Kanuni za Sheria hizo zitawasilishwa haraka iwezekanavyo ili zifanyiwe mapitio na Kamati na kuweza kuishauri Taasisi juu ya Kanuni hizo kwa maslahi mapana ya wananchi.

Aidha, Kamati inachukua fursa hii kuipongeza Serikali na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kwa kufanya marekebisho ya Sheria na sasa tunasubiri Kanuni husika ili hukakikisha Sheria ya Fao la Kuumia Kazini linaekewa utaratibu nzuri wenye ufanisi zaidi katika kusimamia fao hilo.

## USHIRIKISHWAJI WA WADAU

**Mheshimiwa Spika,** licha ya kuwa Kamati imejiridhisha kwamba Kanuni zimefuata taratibu za utungaji lakini kumejitokeza kwa baadhi ya Kanuni kukosekana ushirikishwaji wa Wadau walio wengi wakati wa utungaji wake jambo ambalo ni kasoro kubwa kwa Kanuni hizo hasa ukizingatia kwamba zinagusa maisha ya kila siku ya kila mmoja wetu.

**MAFANIKIO**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati katika kutekeleza kazi yake imepata mafanikio makubwa kwa kukamilisha mizunguko yote iliyopangiwa, kupata mafunzo ambayo yameijenga uwezo Kamati, kuzifanyia mapitio Kanuni zote tulizoziainisha na kupendekeza marekebisho kwa dhamira ya kuziimarisha ili zifikie lengo la kutungwa kwake. Aidha Kamati imefanikiwa kupata mashirikiano makubwa kwa Taasisi zote ambazo Kamati ilihitaji mashirikiano yake.

**CHANGAMOTO**

**Mheshimiwa Spika,** Mbali ya mafanikio yaliyo patikana katika kutekeleza kazi zake pia zimebainika changamoto.

Changamoto kubwa iliyoikabili Kamati nikuwa Kanuni nyingi ziliwasilishwa kwa Lugha ya Kiengereza jambo ambalo lililazimu Kamati kuamuru Kanuni hizo kurudishwa na ziwasilishwe tena zikiwa katika Lugha ya Kiswahili kwani Kiswahili ndio lugha rasmi ya Baraza kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Baraza. Hivyo kuwasilishwa kwa Kanuni kinyume na Katiba ni ukiukwaji wa masharti ya lazima na muktadha huo uwasilishwaji huo ni batili tokea awali (VOID AB INITIO). Aidha Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, 2020, nazo zinasisitiza kuwa lugha ya Kiswahili ndio lugha rasmi ya Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** Ni imani ya Kamati kuwa Kanuni hizo zitawasilishwa tena kwa kufuata utaratibu wa kisheria na kwa lugha rasmi ya Baraza.

**Mapendekezo**

**Mheshimiwa Spika,** katika kutatua changamoto zilizojitokeza kamati inapendekeza yafuatayo:

- Kuwajengea uwezo Watendaji mbali mbali wanaohusika na uandishi wa Kanuni.

- Taasisi ziongeze wigo wa ushirikishwaji wa Wadau katika utungaji wa Kanuni.
- Mamlaka husika zihakikishe kuwa Kanuni zinawasilishwa Barazani zikiwa katika Lugha Rasmi ya Baraza.
- Kamati ipatiwe mafunzo zaidi ya ndani na nje ili kuona Mamlaka nyingine zinavyofanya kazi katika Uchambuzi wa Kanuni na Sheria ndogo ndogo.

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuhitimisha napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Taasisi zifuatazo kwa mashirikiano yao ya hali na mali na kwa muda wao ambavyo kwa pamoja vimepelekea kukamilisha ripoti hii niliyoiwasilisha Taasisi hizo ni:

1. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar,
2. Shirika la Bandari Zanzibar,
3. Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege, Zanzibar,
4. Shirika la Utangazaji Zanzibar,
5. Mamlaka zote za Serikali za Mitaa Zanzibar,
6. Taasisi ya Viwango Zanzibar, na
7. Mwisho ila sio kwa umuhimu Wizara ya Katiba na Sheria, Utumishi na utawala bora Zanzibar.

**Hitimisho**

**Mheshimiwa Spika,** Hivyo, napenda kuhitimisha Muhtasari huu kwa kukushkuru wewe binafsi na Wajumbe wote wa Baraza kwa kunipa muda na usikivu wenu nikaweza kuwasilisha ripoti hii. Aidha ninazishukuru Taasisi ambazo kwa namna moja au nyengine zimefanikisha kukamilika kwa Ripoti hii hususan zile ambazo zimewasilisha Kanuni zao pamoja na Ofisi ya Baraza.

Naomba kutoa hoja.

....................................

Mihayo Juma N'hunga

Mwenyekiti,

Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar**